

# Kukosa ushirikiano chanzo cha utalii kusuasua nchini

Pundamilia na Nyumbu wakiwa kwenye Hifadhi ya Serengeti, Tanzania. **Picha ya Maktaba.**

**TCCIA na CTI, vishirikishe Serikali kupitia BEST-AC kupunguza masharti ya uwekezaji katika sekta ya utalii nchini.**

Veneranda Sumila, Mwananchi

Nchi nyingi zinazoendelea duniani, zimetengeneza sera kuboresha sekta ya utalii kama njia ya kukabiliana na umaskini.

Wataalamu wanasema sera peke yake haiwezi kuboresha sekta ya utalii nchini na kutokana na hali hiyo Serikali inatakiwa kuchukua hatua kadhaa, kuondoa vikwazo vilivyopo katika sekta hiyo kama inataka kuvutia utalii na kuwa namba moja Afrika Mashariki na Bara Afrika.

Moja ya viwakwazo ni sekta hiyo kushindwa kushirikiana na wadau wengine wa utalii.

**Ushirikiano ni muhimu**

Miongoni mwa mambo ambayo yametajwa na wataalamu hao kusaidia kuimarisha sekta ya utalii ni ushirikiano kati ya wadau wa utalii na Serikali.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Wenye Viwanda, Biashara na Kilimo, Tawi la Arusha , Adolf Olomi anaamini kwamba kwa kushirikiana, itapatikana suluhu za changamoto zinazokwamisha sekta hiyo.

Ushirikiano huo pia utasaidia kuwapo kwa mikutano yenye ushawishi kwa Serikali na kuharakisha mchakato wa kuoanisha sheria kwenye itifaki inayoanzisha Soko la Pamoja la Afrika Mashariki (ACCMP).

Utafiti kuhusu utekelezaji wa itifaki ya soko la pamoja nchini Tanzania kwenye sekta ya utalii, wataalamu walishauri wadau katika sekta ya utalii kujenga hoja na kuambatanisha na ushahidi kabla ya kukutana na mamlaka za Serikali ili kupatiwa msaada badala ya kubaki kunung'unika tu.

"Kutegemeana na suala lililopo, Myororo wa Thamani wa Wadau wa Utalii Tanzania (TVC) na wengine wanaofanya shughuli za utalii watafaidika na kushawishi wabunge kuishawishi Serikali kufanya mabadiliko yaliyopendekezwa kwa lengo la kuboresha sekta ya utalii," inasema sehemu ya taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo Tanzania inatakiwa kutengeneza muktadha wa utalii ambao utakuwa ndiyo dira ya miundombinu inayotakiwa kufanikisha sekta ya utalii.

Hali ya sasa si nzuri hasa ukizingatia taarifa ya mwaka 2011 kuhusu utalii duniani na Tanzania imekuwa ni nchi ya 127 kati ya nchi 139 ambazo zina mazingira bora ya utalii ingawa ina vivutio vingi na bora zaidi duniani.

"Ushirikiano kati ya sekta binafsi na umma utasaidia ushawishi kwa Serikali kuona umuhimu wa kuboresha miundombinu ya sekta ya utalii.

"Chama cha biashara ya utalii, kikishirikiana na wadau wengine kama TCCIA na Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI), ni lazima kuishirikisha TPSF kupitia BEST-AC kuangalia namna ya kupunguza changamoto za uwekezaji sekta ya utalii," inasema ripoti ya World Economic Forum ya mwaka 2011.

TVC kupitia nafasi zao ni vyema wakawa na uhusiano wa karibu na BEST – AC, taasisi ya Serikali Ofisi ya Waziri Mkuu yenye lengo la kufanikisha mazingira bora ya kufanyia biashara kwa masilahi ya wajasiriamali, Serikali na walaji.

Uhusiano huo utasaidia kuishawishi Serikali kutekeleza mapendekezo ambayo yameshauriwa katika baadhi ya tafiti mbalimbali zenye lengo la kuboresha sekta ya utalii.

"Pia wadau wa utalii wanaweza kuchambua mawazo ya nchi za Afrika Mashariki kuhusu namna ya kushawishi Serikali kujikita zaidi kutatua changamoto zinazokabili sekta hiyo," inasema ripoti hiyo.

Mbali na hayo umefika wakati TVC kuoanishwa na taarifa ya CIBER ya Desemba 2010 ili kuwa na mfumo wa kudumu wa ushirikiano.

CTI, Tawi la Arusha miaka ya hivi karibuni ilifanya utafiti kuhusiana na TVC na kutoa ripoti ambayo iliyobatizwa CIBER na mapendekezo kadhaa.

"Kwa utekelezaji wa pamoja, kutafanya sekta ya utalii kupanda na kuwa namba mbili kwa vivutio duniani, kushawishi watalii wengi na kupata mapato zaidi," inaeleza ripoti hiyo.

Pamoja na kwamba sekta ya utalii ni ya pili kwa kuingiza fedha za kigeni, sekta hiyo ina tatizo katika uwekezaji na uanzishaji wa shughuli za utalii.

Kwa kuwa huenda itachukua muda mrefu itifaki ya soko la pamoja la Afrika Mashariki kutekelezwa, ni vyema serikali ikafanya mabadiliko yanayotakiwa kwenye sekta ya utalii.

Olomi anasema:"Baadhi ya mambo yanayotakiwa kufanywa, hayana gharama kwa serikali au kupoteza kipato chake, mambo hayo yanarekebisha mwenendo wa sekta ya utalii na kuiweka mahali inapostahili."


**Mathalan nchini Kenya**

Mathalan nchini Kenya mtu anayetaka kuanzisha biashara ya kusafirisha watalii hahitaji kumiliki gari kupewa leseni, lakini Tanzania ni lazima.

Kwa kuwa na utaratibu kama huo hautainyima Serikali mapato kwani mahitaji ya magari yapo na si lazima anayesafirisha watalii kuwa na kampuni bali anaweza kukodisha na kufanya biashara hiyo vizuri.

**Tujadiliane kupitia Ujumbe mfupi SMS kwa 15774 ukianza na neno BIZ na kufuatia ujumbe wako. Ujumbe wako mfupi ni Bure, hautozwi.**

**HABARI ZAIDI**



**-Sera ya utalii, sheria ya utalii na kanuni zake zinatakiwa kupitiwa upya.**

**-Kanuni zinazosimamia utalii kabla ya kuanza kufanyakazi, uhusiano wake uangaliwe upya pia.**

**-Eneo maalumu litengwe na kutumika kwa ajili ya malipo ya kodi ushuru na kadhalika.**

**-Sekta ya umma na binafsi ziishawishi Serikali na mamlaka nyingine kuboresha miundombinu kwenye sekta ya utalii.**

BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy
UKURASA HUU UNADHAMINIWA NA BEST-AC NA MWANANCHI